

Swahili transcript:

Mimi nimeolewa, mimi niliolewa mwaka wa 2000, ilikuwa ni tarehe tisa mwezi wa kumi na mbili, na kwa sasa namshukuru Mungu nina watoto wawili, mtoto wa kwanza ni wa kiume anaitwa Hezekiah, na mtoto wa pili ni wa kike anaitwa Keziah, na ndio hao ambao mimi na mume wangu mpenzi Sixfrid Jacob tulikuwa tumepanga tuwe na watoto wawili, ili kwamba tuweze kuwahudumia vizuri, tuweze kuwapa mahitaji yao, ili waweze kuishi vizuri, waweze kula vizuri, waweze kuvaa vizuri na waweze kwenda shule nzuri ili waweze kuja kuwa na maisha mazuri hapo baadae. Kwa hiyo suala zima la uzazi wa mpango na katika mambo ya uzazi, watazania sasa wamegeuka, aah! si kawaida tena kwa miaka ya hivi karibuni kukuta familia watu wanazaa labda watoto saba au kumi, hapana, saa hizi katika ndoa nyingi za hivi karibuni, miaka ya tisini mpaka elfu mbili utakuta watu wanazaa mtoto mmoja, au watoto wawili au wengi wamezidi sana watoto watatu. Na jambo hili limeenea sasa mpaka vijijini pia nao wamepata uelewa kwamba wanatakiwa wazae watoto ambao wataweza kuwatunza vizuri, na kuwahudumia vizuri katika maisha yao. Kwa hiyo, kwa hilo pia tunaipongeza serikali ya Tanzania kwa kweli wamejitahidi katika kuielimisha jamii na kwa sasa Tanzania wanazaa watoto ambao wataweza kuwasomesha vizuri, wataweza kuwatunza vizuri na kuwaandaa vizuri katika maisha yao ya baadae.

English translation:

I was married on December 9th, 2000. I thank God, for now I have two children. The firstborn is a son, called Hezekiah, and the second born is a daughter, called Keziah. These are the ones I and my beloved husband Sixfrid Jacob planned to have. We planned these two children so that we could manage to take care of them, by buying them good clothes, giving them good food, and sending them to good schools. In the future, they will live better. By now, most Tanzanian families have a good understanding of family planning. It is unusual to find a family that has seven or ten children the way it was in the

past. Not at all! In recent marriages, say, from the nineties to 2000, people have had one or two children, and if any more than that, then maybe three. The family planning program has reached many people, even in rural areas. They understand that they should only bear children they will be able to care for. We congratulate our government for the massive effort to teach Tanzanians about family planning. For now, Tanzanians will be able to send their children to school, to care for them and to prepare them for a better future.

About CultureTalk: CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated